

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO

15 MEI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO – TAREHE 15 MEI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**317. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES
WAMBURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Shule ya Sekondari Mkalapa itatambuliwa kuwa Shule ya vipaji vya michezo ya mpira wa wavu.

**318. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY
(MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ujenzi wa Maabara za Sayansi katika Shule za Sekondari utakamilika kama ilivyokusudiwa katika Bajeti ya 2022/2023.

**319. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA
HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Iyula – Ipyana hadi Idunda - Vwawa.

**320. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI
(UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Mamlaka ya Mji Mdogo wa Nansio haifanyi kazi.

WIZARA YA AFYA:

**321. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na ongezeko la Wagonjwa wa Kansa ya Kizazi.

**322. MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha huduma za *dialysis* kwa Wagonjwa wenye kipato cha chini.

**323. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itaongeza Wauguzi katika Hospitali ya Bugando kwani kwa sasa ina upungufu wa Wauguzi 1,200.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**324. MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha ukusanyaji Mapato kwa Biashara zinazofanyika Mtandaoni.

WIZARA YA KILIMO:

**325. MHESHIMIWA DKT. ALFRED JAMES KIMEA
(KOROGWE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga miundombinu ya umwagiliaji katika Mabonde ya Mpunga ya Mahenge, Goo na Kwamngumi - Korogwe Mjini.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

**326. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER
CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa nyumba za Watumishi nchini hasa katika Halmashauri mpya.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**327. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ipo tayari kuruhusu uraia pacha kwa Watanzania wenye uraia wa nchi nyingine.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**328. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA
(MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya mchepuko ya Mlima Nyoka (Uyole) hadi Uwanja wa Ndege Songwe.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**329. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE
(KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itajenga Soko la Samaki Kilwa Kivinje.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**330. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN
MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Mahakama ya Wilaya ya Nyasa itaanza kujengwa.

WIZARA YA MAJI:

**331. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY
MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatatua tatizo la ukosefu wa maji katika Jimbo la Mbogwe.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA AFYA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
15 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

